**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**

Simu: 022-2121600
Faksi: 022-2113271 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Tz
Tovuti: www.moe.go.tz

## NAFASI ZA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA CHETI NA STASHAHADA: JULAI 2008/2009

Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi anatangaza nafasi za mafunzo ya ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada kama ifuatavyo:

**A: Maelekezo muhimu kwa waombaji:**

(i) Waombaji wa Mafunzo ya Ualimu ngazi ya Cheti (IIIA) watachaguliwa kupitia "**Selforms**". Hata hivyo watapaswa kuthibitisha kwa barua. Aidha maombi binafsi yatafikiriwa pia. Watakaohusika ni wahitimu wa kidato cha IV waliohitimu mwaka 2007 wenye ufaulu usiopungua Divisheni IV alama 28.

(ii) Waombaji wa Mafunzo ya Ualimu ngazi ya Stashahada wawe wamehitimu kidato cha VI kati ya mwaka 2000 na 2007 na wawe na ufaulu usiopungua 'Principal Pass' moja na 'Subsidiary' moja.

(iii) Muda wa mafunzo ni miaka miwili na mafunzo yataanza Julai 2008.

(iv) Maombi yaambatane na nakala za vyeti vya Kidato cha IV, Kidato cha VI na Cheti cha Ualimu kwa wale ambao ni walimu. Aidha maombi yaambatane na picha mbili za mwombaji (passport size).

(v) Maombi yaoneshe kiwango cha taaluma, ufaulu wa kila somo katika mtihani wa mwisho na umri wa mwombaji. Aidha mwombaji aoneshe ni mwanamme / mwanamke na umri kazini kwa wale walioajiriwa.

(vi) Upo uwezekano wa kupata mafunzo ya ualimu mwanafunzi akiwa anaishi nje ya chuo. Endapo mwombaji atapenda kusoma akiwa nje ya chuo aeleze na ataje chuo anachopendelea kusoma.

(vii) Barua za waombaji wa Mafunzo ya Walimu Kazini zipitishwe kwa waajiri.

**(viii) Maombi yenye anuani nje ya Dar es Salaam, na yenye uthibitisho wa kuwa tayari kufundisha katika wilaya ambazo kwa kawaida zina upungufu mkubwa wa walimu yatafikiriwa KWANZA.**

**B: Kuajiriwa baada ya mafunzo:**

(i) Wahitimu wa Mafunzo ya Ualimu (tarajali) ngazi ya Cheti na Stashahada wana nafasi ya kuajiriwa serikalini.

(ii) Wahitimu wa Mafunzo ya Ualimu (Kazini) ngazi ya Stashahada Elimu Maalum, Sayansi Kimu, Sanaa, Ufundi, Maonesho, Muziki na Michezo ambao wana ajira watarudi kwa waajiri wao kufundisha fani walizosomea.

**C**: **Gharama za mafunzo**: Ada kwa Mafunzo ya Ualimu (tarajali) ngazi ya Cheti (IIIA) na Stashahada (tarajali na mafunzo kazini) kwa kila mwaka wa masomo ni **shs. 150,000/=.**

**D: Aina ya mafunzo yatakayotolewa na sifa zinazotakiwa ni kama ifuatavyo:**

| NA | MAFUNZO | SIFA ZA WAOMBAJI |
|---|---|---|
| 1. | Stashahada ya Ualimu (tarajali):<br>Muda wa mafunzo miaka 2. | Awe amefaulu kidato cha VI kwa kiwango kisichopungua 'Principal Pass' moja na 'subsidiary' moja katika masomo yanayofundishwa shule za sekondari**. AU** awe na cheti cha FTC katika masomo ya Sayansi na Hisabati. |
| 2. | Stashahada ya Ualimu (kazini):<br>Muda wa mafunzo miaka 2. | (a) Awe mwalimu anayefundisha na mwenye Cheti cha Ualimu (IIIA) na uzoefu kazini usiopungua miaka mitatu.<br>(b) Awe amefaulu Kidato cha Sita kwa kiwango kisichopungua 'Principal Pass' moja na 'subsidiary' moja katika masomo yanayofundishwa shule za sekondari. |
| 3. | Stashahada ya Ualimu (Elimu Maalum):<br>Muda wa mafunzo miaka 2. | (a) Awe mwalimu mwenye Cheti cha Ualimu (IIIA) cha Elimu Maalum, na ambaye amefaulu masomo mawili Kidato cha Sita. **AU**<br>(b) Awe mwalimu mwenye Stashahada ya Ualimu fani ya Sayansi/Sayansi ya Jamii na awe na uzoefu kazini usiopungua miaka 3. Aina ya mafunzo: (i) Wasioona (ii) Viziwi (iii) Watoto wenye ulemavu wa akili.<br>(c) Awe ameshinda Kidato cha VI kwa kiwango kisichopungua 'Principal Pass' moja na 'subsidiary' moja na anapenda kufundisha watoto wenye mahitaji maalum (wasioona, viziwi, watoto wenye ulemavu wa akili). |
| 4. | Stashahada ya Ualimu Sayansi kimu:<br>Muda wa mafunzo miaka 2. | (a) Awe mwalimu mwenye Cheti cha: Ualimu Daraja IIIA, Sayansi Kimu na awe ameshinda kwa kiwango kisichopungua "Principal Pass" moja na "Subsidiary" moja katika masomo ya: Baiyolojia, Kemia na Sayansi Kimu katika mitihani ya Kidato cha VI. **AU**<br>(b) Awe ameshinda kwa kiwango kisichopungua "Principal Pass" moja na "Subsidiary" moja katika mitihani Kidato cha VI katika masomo ya Sayansi Kimu na somo mojawapo kati ya: Baiyolojia, Kemia, Kilimo, Fizikia, Hisabati, 'Textile' na 'Nutrition'. |
| 5. | Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu (Michezo, Muziki, Sanaa Maonesho/Ufundi).<br>Muda wa mafunzo miaka 2. | (a) Awe mwalimu mwenye cheti cha Ualimu Daraja IIIA na aliyejiendeleza hadi Kidato cha Sita na kufaulu kwa kiwango kisichopungua ''Principal Pass'' moja na "Subsidiary" moja. Kozi ya **Sanaa za Maonesho,** afaulu katika masomo yanayostahili: English literature, Kiswahili, Jiografia na Historia. Kozi ya **Muziki,** afaulu katika masomo yanayostahili: English, Kiswahili, Muziki, Historia, Jiografia na Fizikia. Kozi ya **Sanaa Ufundi,** afaulu katika masomo yanayostahili: "Fine Art" na /au masomo mengine yanayoendana na kozi yenyewe. Kozi ya **Elimu kwa Michezo,** afaulu katika masomo yanayostahili: Baiyolojia, Kemia, Fizikia, English na Kiswahili.<br>**AU**<br>(b) Awe ameshinda Kidato cha VI kwa kiwango kisichopungua "Principal Pass" moja na "Subsidiary" moja katika masomo yaliyotajwa hapo juu na kuonyesha uwezo, stadi, na mwelekeo katika fani anayoomba.<br>(c) Waombaji wote watakaochaguliwa watafanyiwa usaili chuoni kabla ya kujiunga na mafunzo. |

| NA | MAFUNZO | SIFA ZA WAOMBAJI |
|---|---|---|
| 6. | Mafunzo ya Cheti cha Ualimu (Sayansi Kimu):<br>Muda wa mafunzo mwaka 1. | (a) Awe mwalimu mwenye Cheti cha Ualimu Daraja IIIA.<br>(b) Awe na uzoefu kazini usiopungua miaka 3.<br>(c) Awe amefaulu katika mtihani wa kidato cha IV masomo ya Sayansi Kimu au Masomo ya Sayansi. |
| 7. | Mafunzo ya Cheti cha Ualimu (Elimu Maalum):<br>Muda wa mafunzo mwaka 1. | (a) Awe mwalimu mwenye cheti cha ualimu daraja la IIIA.<br>(b) Awe amefundisha kwa muda usiopungua miaka 3.<br>(c) Awe amefaulu masomo ya Sayansi katika mitihani ya kidato cha Nne.<br>(d) Awe mwalimu anayefundisha Elimu Maalum bila mafunzo rasmi. |
| 8. | Stashahada (Technical Education.)Muda wa mafunzo miaka 2 | Awe amefaulu na kupata cheti cha FTC kutoka vyuo vya Ufundi Arusha, Mbeya, Dar es Salaam au sifa inayolingana. |
| 9. | Stashahada (Agriculture Education) | Awe amefaulu kidato cha VI kiwango cha angalau “Principal Pass” moja na “Subsidiary” moja katika masomo ya Baiyologia na Kilimo au sifa inayolingana. |
| 10. | Stashahada (Commerce/Acauntancy) | Awe amefaulu kidato cha VI, kiwango kisichopungua “Principal Pass” moja na “Siubsidiary’” moja katika masomo ya Biashara na Uhasibu. |

**E. Angalizo; waombaji wenye ufaulu katika masomo ya Hisabati, Lugha (Kiswahili, “English”, “French”) na Sayansi watapewa kipaumbele.**

**F. Waombaji wenye anuani nje ya Dar es Salaam na wanaotoka wilaya ambazo kwa kawaida zina upungufu mkubwa wa walimu watafikiriwa kwanza. Mikoa/Wilaya hizo ni pamoja na: Shinyanga, Singida, Tabora, Lindi, Mtwara, Kigoma, Rukwa, Pwani (Mafia, Rufiji), Manyara (Kiteto, Simanjiro), Arusha (Ngorongoro), Morogoro (Ulanga), Ruvuma, Kagera (Biharamulo), Mara (Musoma Vijijini, Tarime, Serengeti), Mwanza, Tanga (Handeni, Kilindi, Lushoto), Dodoma (Kongwa, Kondoa, Bahi).**

**Maombi haya yatapaswa kupata uthibitisho usio na mashaka kutoka kwa Maafisa Elimu (W).**

**G: Maombi yote yatumwe kwa kutumia anuani ifuatayo:**
KATIBU MKUU,
WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI,
S.L.P. 9121,
**DAR ES SALAAM. (Aione Mkurugenzi, Elimu ya Ualimu).**

**MAJIBU YATATOLEWA KWA WATAKAOTEULIWA TU.**
**MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI NI TAREHE 15/05/2008.**

**LIMETOLEWA NA: KATIBU MKUU, WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**
**S.L.P. 9121 DAR ES SALAAM**